**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: COMP-2024-00000270**
**NAMBA YA LOIS: GA.71/135/EZ/2024/14**

**KATI YA**

**PROCHES E. SWAI, ZUBERI ALLY NA**
**ISSA HASSAN ............................................................................ WALALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ......................... MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 144 cha tarehe 17 Januari 2025)***

## 3.0 Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 05 Novemba 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Proches E. Swai, Bw. Zuberi Ally na Bw. Issa Hassan wa Kibaha (Walalamikaji) dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) (Mlalamikiwa). Walalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kushindwa kuwapatia huduma ya umeme eneo la Kwa Mfipa Mkoani Kibaha.

Walalamikaji wanaeleza kwamba waliomba kuunganishiwa miundombinu ya umeme mwaka 2021 kutoka ofisi ya Mlalamikiwa na mnamo mwaka 2023, Mlalamikiwa alianza kutekeleza baadhi ya maombi ya walalamikaji kwa njia ya kuweka mradi wa usimikaji wa nguzo kwa ajili ya usambazaji wa umeme katika eneo linalolalamikiwa.

Walalamikaji wanaeleza kwamba Mlalamikiwa alitekeleza baadhi ya sehemu ya mradi ambao waliahidiwa, lakini baada ya kutekeleza sehemu ndogo ya mradi huo, ofisi ya Mlalamikiwa kupitia maofisa wake walianza kuhamisha baadhi ya vifaa ambavyo vipo eneo linalolalamikiwa wakiashiria kumalizika kwa mradi huo. Walalamikaji wanaeleza walifika ofisi ya Mlalamikiwa na kuulizia mwendelezo wa mradi wa usambazaji wa umeme katika eneo lao lakini hawakupata majibu yanayoridhisha. Hivyo waliamua kuwasilisha malalamiko yao ofisi ya Mlalamikiwa kwa lengo la kupata muafaka wa malalamiko yao.

Mnamo tarehe 05 Novemba 2024 Walalamikaji waliwasilisha malalamiko yao kwa Mamlaka (EWURA) na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa kuwapatia huduma ya umeme katika eneo linalolalamikiwa na mradi ulioanza kutekelezwa umalizwe.

Baada ya kupokea malalamiko ya Walalamikaji, Mamlaka (EWURA) mnamo tarehe 28 Oktoba 2024, ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuleta waraka wa utetezi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Utatuzi wa MigogoroTS Na. 428/2020.

Mnamo tarehe 26 Novemba 2024, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Walalamikaji na kueleza kwamba bado wanaendelea kutekeleza mradi wa umeme katika eneo lalamikiwa na hivyo Walalamikaji watapata huduma ya umeme mara baada ya kukamilisha mradi huo wa umeme. Mlalamikiwa anaendelea kueleza kwamba Walalamikaji wanastahili kupata huduma ya umeme.

Kikao cha usuluhishi baina ya pande zote mbili kilifanyika tarehe 17 Disemba 2024, katika hoteli ya Njuweni Mkoa wa Pwani na katika majadiliano baina ya pande mbili mwisho wa kikao cha usuluhishi muafaka ulifikiwa kwa makubaliano yafuatayo:-

(i) kwamba Mlalamikiwa ataweka nguzo kumi na tatu (13) za njia ya umeme mdogo kwa muda wa siku 75 kuanzia tarehe 17 Disemba 2024 hadi tarehe 28 Februari 2025; na
(ii) kwamba Walalamikaji watafuta nafuu zao zote mara baada Mlalamikiwa atakapo weka nguzo kumi na tatu kwa muda wa siku 75 kuanzia tarehe 17 Disemba 2024 hadi tarehe 28 Februari 2025.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali Na. 428 la 2020 na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 4.0 Makubaliano

Pande zote mbili zilikubaliana yafuatayo:-

(a) Mlalamikiwa ataweka nguzo kumi na tatu za njia ya umeme mdogo kwa muda wa siku 75 kuanzia tarehe 17 Disemba 2024 hadi tarehe 28 Februari 2025; na
(b) Walalamikaji watafuta nafuu zao zote mara baada Mlalamikiwa mlalamikiwa atakapo weka nguzo kumi na tatu kwa muda wa siku 75 kuanzia tarehe 17 Disemba 2024 hadi tarehe 28 Februari 2025.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali namba 428 la 2020, makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Dodoma tarehe 17 mwezi Januari 2025.

..............................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**